TANGAZO LA SERIKALI Na. 490 la tarehe. 14/6/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA USHURU WA MAZAO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"gulio" maana yake ni eneo maalumu au sehemu yoyote ya wazi au iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli za kuuza na kununua mazao ya nafaka, misitu au bidhaa za viwandani kwa siku maalum;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa;

"lumbesa" maana yake ni ufungashaji wa bidhaa za mazao kwa ujazo usiozingatia vipimo sahihi katika magunia au vifungashio;

"mazao" maana yake ni mavuno yanayotokana na kilimo, misitu au uvuvi yanayozalishwa katika eneo la Halmashauri;

"mfanyabiashara" maana yake ni mtu binafsi, taasisi, kampuni au kikundi cha watu wanaojishughulisha na shughuli za kuuza na kununua bidhaa au mazao kwa lengo la kupata faida;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnunuzi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au shirika lolote linalonunua bidhaa au mazao katika eneo la Halmashauri;

"muuzaji" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au shirika linalouza mazao katika eneo lililoidhinishwa na Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kampuni, kikundi cha watu au shirika lililoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Ushuru wa mazao

4. -(1) Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa mazao yatakayozalishwa katika eneo la Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Ushuru wa mazao utalipwa na mnunuzi kwa kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hii.

(3) Baada ya kulipa ushuru mnunuzi atapewa stakabadhi ya malipo na atawajibika kuionesha kwa Afisa Mwidhiniwa atakapotakiwa kufanya hivyo.

(4) Stakabadhi zitakazotolewa kwa malipo ya ushuru wa mazao zitakuwa za kielektroniki.

(5) Malipo yote yatafanywa kwa Afisa Mwidhiniwa, benki au kwa Wakala atakayekuwa ameteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kazi hiyo.

Matumizi ya vipimo sahihi vya mazao

5. -(1) Upimaji wa mazao utafanyika kwa mizani au kipimo chochote kingine kilichothibitishwa na Halmashauri au mamlaka nyingine iliyowekwa kisheria.

(2) Mtu hataruhusiwa kufunga, kuuza au kusafirisha mazao yaliyofungwa kwa lumbesa.

(3) Mnunuzi hataruhusiwa kupokea au kusafirisha mazao ambayo hayajalipiwa ushuru kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hii.

Uteuzi wa Wakala

6. Halmashauri inaweza kumteaua mtu binafsi, kikundi,

kampuni au taasisi kuwa Wakala wa kukusanya ushuru chini ya Sheria Ndogo hii na Wakala huyo atawajibika kutekeleza masharti yote ya kutoza ushuru yaliyoainishwa na Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa Wakala

7. Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 6 atakuwa na wajibu wa-
(a) kuwasilisha kwa Halmashauri kiasi cha ushuru alioukusanya;
(b) kukusanya ushuru kwa kiwango kilichoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;
(c) kutoa taarifa kwa Halmashauri kuhusiana na mtu yeyote ambaye amekataa au anakwepa kulipa ushuru; na
(d) kuishauri Halmashauri namna ya kuboresha ukusanyaji wa ushuru.

Rejesta ya wanunuzi wa mazao

8. (1) Halmashauri itakuwa na Rejesta maalumu ya orodha ya wanunuzi wa mazao ndani ya eneo la Halmashauri na itakuwa ni wajibu wa kila mnunuzi kuhakikisha amejiandikisha kwenye rejesta hiyo.

(2) Kila kijiji kitawajibika kutunza Rejesta yake kwa ajili ya kumbukumbu ya wanunuzi wa mazao kwenye eneo lake.

Leseni ya biashara

9. Mfanyabiashara atatakiwa kuwa na leseni ya biashara pamoja na kibali toka Halmashauri kitakachomruhusu kufanya biashara katika eneo la Halmashauri.

Ushuru wa mazao ya misitu

10. -(1) Halmashauri itatoza ushuru kwa mazao ya misitu yatakayosafirishwa ndani na nje ya Halmashauri kwa viwango vilivyoorodheshwa katika Jedwali la Pili.

(2) Ushuru wa mazao utalipwa kwa Afisa Mwidhiniwa au Wakala aliyeteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri na utalipwa kabla ya mnunuzi kusafirisha mazao yake.

(3) Mnunuzi hataruhusiwa kusafirisha mazao ya misitu bila kuwa na kibali maalumu kwa shughuli hiyo.

(4) Kibali kitaonesha jina la mnunuzi, aina ya mazao aliyonunua, sehemu yaliponunuliwa na maoni ya Halmashauri.

Ushuru wa uvuvi wa samaki

11.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa uvuvi wa samaki watakaovuliwa katika mabwawa yaliyopo ndani ya eneo lake kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(2) Samaki wabichi na waliokaushwa watapimwa katika mizani ili kupata uzito kabla ya kulipiwa ushuru.

Uanzishaji wa masoko

12. Kila kijiji ndani ya Halmashauri kitatenga eneo maalumu kwa ajili ya biashara ya bidhaa au mazao na kila mfanyabiashara atauzia bidhaa au mazao yake katika eneo hilo.

Ushuru wa trekta

13.-(1) Kila trekta litakaloingizwa au kutumika kwa shughuli za kilimo katika eneo la Halmashauri litapaswa kuombewa kibali na kulipiwa ushuru.

(2) Kibali kitatolewa na Afisa Mwidhiniwa, mtendaji wa Kata au mtendaji wa Kijiji.

(3) Malipo ya ushuru wa trekta yatafanyika kwa kila msimu wa kilimo na yatakuwa katika kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Nne.

Muda wa Kusafirisha mazao

14. -(1) Mnunuzi atatakiwa kusafirisha mazao kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.

(2) Mnunuzi atakayesafirisha mazao kinyume na muda ulioainishwa chini ya kanuni ndogo ya (1) atapaswa kuomba kibali kwa mtendaji wa kijiji au kata na kabla ya kuomba kibali hicho awe amelipia ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa

15.-(1) Mnunuzi anatenda kosa ikiwa

(a) anasafirisha mazao yaliyonunuliwa kabla ya kulipa ushuru;
(b) anasafirisha mazao wakati wa usiku;
(c) anasafirisha mazao bila kulipia ushuru;
(d) ananunua mazao bila kuwa na leseni na kibali; au
(e) anakataa kuonesha stakabadhi ya malipo aliyolipia ushuru kwa Afisa Mwidhiniwa;
(f) anampa mtu, kampuni, taasisi, kikundi au Wakala mwingine kibali chake; au
(g) anafungasha au kusafirisha mazao katika mtindo wa lumbesa.

(2) Muuzaji anatenda kosa ikiwa-

(a) anauza mazao katika maeneo yasiyoruhusiwa au

kutengwa kwa shughuli hiyo; au

(b) anafanya jambo lolote litakalosababisha Mnunuzi kukwepa kulipa Ushuru.

(3) Wakala anatenda kosa ikiwa-

(a) anachelewa kuwasilisha ushuru kwa Halmashauri;

(b) anatoa taarifa za uongo kuhusu idadi ya watu, kampuni au taasisi wanaolipa Ushuru na thamani yake;

(c) anawasilisha kwa Halmashauri kiwango kidogo cha fedha kinyume na makubaliano; au

(d) anamshawishi mtu, kikundi, kampuni au taasisi kutolipa ushuru.

Adhabu.

16. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha kosa

17. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa T. S Na.177 la 2013

18. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa za Mwaka, 2013 zinafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

USHURU WA MAZAO

| NA. | AINA YA MAZAO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | Tshs. 1,000/= Kwa gunia la Kg 100 |
| 2. | Alizeti | Tshs. 1,000/= Kwa gunia la Kg 65 |
| 3. | Ufuta | Tshs. 1,500/= Kwa gunia la Kg 100 |
| 4. | Maharage | Tshs. 2,000/= Kwa gunia la Kg 100 |
| 5. | Karanga | Tshs. 1,000/= Kwa gunia la Kg 100 |
| 6. | Dengu | Tshs. 2,000/= kwa gunia la Kilo 100 |
| 7. | Mbaazi | Tshs. 2,000/= kwa gunia la Kilo 100 |
| 8. | Kunde | Tshs. 1,000/= kwa gunia la Kilo 100 |
| 9. | Mtama | Tshs. 1,000/= Kwa gunia la Kg 100 |
| 10. | Miwa | Tshs. 6,000/= Kwa kila tani |
| 11. | Ndizi | Tshs. 500/= Kwa Mkungu |
| 12. | Mihogo | Tshs. 1,000/= kwa kiroba |
| 13. | Vitunguu | Tshs. 1,500/= kwa gunia |
| 14. | Nyanya | Tshs. 1,000/= kwa tenga |
| 15. | Mazao mengine | Tshs. 200/= Kwa gunia la Kg 100 |
| 16. | Mafuta ya Alizeti | Tshs. 1,000/=kwa Ndoo ya Lita 20 |
| 17. | Mashudu | Tshs. 500/= kwa gunia |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10(1))*

USHURU WA MAZAO YA MISITU

| NA. | AINA YA BIDHAA | UJAZO | USHURU |
|---|---|---|---|
| 1. | Mbao za miti migumu | Kila ubao mmoja | Tshs. 2,000/= |
| 2. | Mbao za miti laini | Kila ubao mmoja | Tshs. 1,000/= |
| 3. | Mkaa | Gunia moja | Tshs. 2,000/= |
| 4. | Asali | Kwa kila -Lita 20 | Tshs. 5,000/= |
| 5. | Nta | Kwa Ndoo ya Lita 20 | Tshs. 500/= |

## JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 11(1))*

USHURU WA MAZAO YA UVUVI NA SAMAKI

| NA. | AINA YA USHURU | KIASI CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa Samaki Wabichi | Tshs. 500/= kwa kilo |
| 2. | Ushuru wa Samaki wakavu | Tshs. 300/= kwa kilo |

## JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini kanuni ya 13(3))*

USHURU WA TREKTA

| NA | AINA YA USHURU | KIASI CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa kuingiza Trekta kwa shughuli za kilimo | Tshs. 30,000/= kwa msimu wa Kilimo |

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 17)*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi .....................................................wa S.L.P ................................. Namba ya Simu: .................................. Nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya .............................. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, kwamba mnamo tarehe ..................ya Mwezi ......................... Mwaka ..................... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya .................. ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ya Mwaka 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha ada/ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe .......................................ya Mwezi.................................Mwaka.........................
Jina::........................................................ Saini:........................................................................

MBELE YA:
Jina:...............................................................
Cheo:...........................................................
Saini:............................................................

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa uliofanyika tarehe 28/4/2022 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

SHABANI KAPALA MILLAO,
*Mkurugenzi Mtendaji (w),*
*Halmashauri ya Wilaya Kondoa*

ABDALLAH SALUM MAGUO,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya Kondoa*

**NAKUBALI**,

L.S

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-Tamisemi*